



Scriptures taken from Kiswahili Contemporary Version
Copyright (c) 1984, 1989, 2006 by International Bible Society(R)
Used by permission. All rights reserved worldwide.



Taken from The Holy Bible, English Standard Version 
copyright (c) 2001 by Crossway Bibles,
a division of Good News Publishers.
Used by permission. All rights reserved.

Neno Aprili 2014

The Word April 2014

Kiswahili Contemporary Version 2006
English Standard Version



Project Bible 2.0 www.bible2.net

Neno la Jumanne, 29. Aprili 2014

Yesu akasema:
Mimi na Baba Yangu tu Umoja.
Yohana 10,30

Paulo akaandika:
Ikamilisheni furaha yangu kwa kuwa na nia kama hiyo,
mkiwa na upendo huo huo,
wenye roho moja na kusudi moja.
Wafilipi 2,2

Jesus said:
I and the Father are one.
John 10:30 (ESV)

Paul writes:
Complete my joy by being of the same mind,
having the same love,
being in full accord and of one mind.
Philippians 2:2

Neno la Jumatano, 2. Aprili 2014

Wote wamepotoka, wameoza wote pamoja,
hakuna atendaye mema, naam! Hata mmoja.
Zaburi 14,3

Heri mtu yule ambaye BWANA
hamwesabii dhambi na ambaye
rohoni mwake hamna udanganyifu.
Zaburi 32,2

They have all turned aside;
together they have become corrupt;
there is none who does good, not even one.
Psalms 14:3 (ESV)

Blessed is the man against whom the Lord counts no
iniquity,
and in whose spirit there is no deceit.
Psalms 32:2 (ESV)

Neno la Jumapili, 27. Aprili 2014

Roho wa BWANA Mwenyezi yu juu yangu,
kwa sababu amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari
njema.

Amenituma kuwaganga waliovunjika moyo,
kuwatangazia mateka uhuru wao
na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao.

Isaya 61,1

Petro akawekwa gerezani,
lakini kanisa lilikuwa likimwomba kwa Mungu kwa bidii.

Matendo ya Mitume 12,5

The Spirit of the Lord God is upon me,
because the Lord has anointed me
to bring good news to the poor;
he has sent me to bind up the brokenhearted,
to proclaim liberty to the captives,
and the opening of the prison to those who are bound.

Isaiah 61:1 (ESV)

Peter was kept in prison,
but earnest prayer for him was made to God by the church.

Acts 12:5 (ESV)

Neno la Ijumaa, 25. Aprili 2014

Ni mtu gani awezaye kuishi na asione kifo,
au kujiokoa mwenyewe kutoka nguvu za kaburi?

Zaburi 89,48

Malaika akawaambia wanawake:

Hayupo hapa, kwa kuwa amefufuka, kama vile alivyosema.
Njoni mpatazame mahali alipokuwa amelazwa.

Mathayo 28,6

What man can live and never see death?
Who can deliver his soul from the power of Sheol?

Psalms 89:48 (ESV)

The angel of the Lord said to the women:

He is not here, for he has risen, as he said.

Come, see the place where he lay.

Matthew 28:6 (ESV)

Neno la Ijumaa, 4. Aprili 2014

Usiwe mbali nami,
kwa maana shida iko karibu na hakuna wa kunisaidia.

Zaburi 22,11

BWANA yu karibu nao waliovunjika
moyo na huwaokoa waliopondeka roho.

Zaburi 34,18

Be not far from me,
for trouble is near,
and there is none to help.

Psalms 22:11

The Lord is near to the brokenhearted
and saves the crushed in spirit.

Psalms 34:18

Neno la Jumapili, 6. Aprili 2014

Uwe imara na hodari sana. Usiogope wala usivunjike
moyo,
kwa kuwa BWANA wako, atakuwa pamoja nawe ko kote
uendako.

YOSHUA 1,9

Msiwaogope wale wauao mwili lakini hawawezi kuua roho
afadhali

mwogopeni yeye awezaye kuiangamiza roho na mwili
katika jehanam.

Mathayo 10,28

Do not be frightened, and do not be dismayed,
for the Lord your God is with you wherever you go.

Joshua 1:9 (ESV)

Do not fear those who kill the body but cannot kill the soul.
Rather fear him who can destroy both soul and body in
hell.

Matthew 10:28 (ESV)

Neno la Jumatano, 23. Aprili 2014

Usiogope, Abram.
Mimi ni ngao yako na
thawabu yako kubwa sana.
Mwanzo 15,1

Mungu si dhalimu, hataisahau kazi yenu na upendo
ule mlioonyesha kwa ajili Yake katika kuwahudumia
watakatifu
na kama vile mnavyoendelea kuwahudumia.
Waebrania 6,10

Fear not, Abram, I am your shield;
your reward shall be very great.
Genesis 15:1 (ESV)

God is not unjust so as to overlook your work
and the love that you have shown for his name
in serving the saints, as you still do.
Hebrews 6:10

Neno la Jumatatu, 21. Aprili 2014

Msifuni BWANA.
Heri mtu yule amchaye BWANA,
mtu yule apendezwaye sana na amri zake.
Zaburi 112,1

Bali wenye haki na wafurahi washangilie mbele za Mungu,
na wafurahi na kushangilia.
Zaburi 68,3

Blessed is the man who fears the Lord,
who greatly delights in his commandments!
Psalms 112:1

The righteous shall be glad;
they shall exult before God;
they shall be jubilant with joy!
Psalms 68:3 (ESV)

Neno la Jumanne, 8. Aprili 2014

Thomasi akamwambia,
“Bwana, sisi hatujui unakokwenda, tutaijuaje njia?”
Yohana 14,5

Wewe ni taa yangu, Ee BWANA.
BWANA hulifanya giza langu kuwa mwanga.
2 Samweli 22,29

Thomas said to Jesus,
Lord, we do not know where you are going.
How can we know the way?
John 14:5

You are my lamp, O Lord,
and my God lightens my darkness.
2 Samuel 22:29 (ESV)

Neno la Alhamisi, 10. Aprili 2014

Nilipojaribu kuelewa haya yote, yalikuwa magumu kwangu
kuelewa.

Mpaka nilipoingia mahali patakatifu pa Mungu,
ndipo nilipotambua mwisho wao.
Zaburi 73,16-17

Usitishwe mtu anapotajirika,
fahari ya nyumba yake inapoogezeka,
kwa maana hatachukua cho chote atakapokufa,
fahari yake haitashuka pamoja naye.
Zaburi 49,16-17

When I thought how to understand this,
it seemed to me a wearisome task,
until I went into the sanctuary of God;
then I discerned their end.
Psalms 73:16-17 (ESV)

Be not afraid when a man becomes rich,
when the glory of his house increases.
For when he dies he will carry nothing away;
his glory will not go down after him.
Psalms 49:16-17 (ESV)

Neno la Jumamosi, 19. Aprili 2014

Kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao
alidharauliwa,
wala hatukumhesabu kuwa kitu.
Isaya 53,3

Alikuja kwa walio Wake, lakini wao hawakumpokea.
Yohana 1,11

As one from whom men hide their faces
he was despised, and we esteemed him not.
Isaiah 53:3 (ESV)

He came to his own,
and his own people did not receive him.
John 1:11 (ESV)

Neno la Alhamisi, 17. Aprili 2014

Hakika alichukua udhaifu wetu na akajitwika huzuni zetu,
hata hivyo tulifikiri amepigwa na Mungu,
amepigwa sana naye na kuteswa.
Isaya 53,4

Yesu akiwa ameubeba msalaba Wake,
akatoka kuelekea mahali palipoitwa,
'Fuvu la Kichwa,' au ambapo kwa Kiebrania ni Golgotha.
Yohana 19,17

Surely he has borne our griefs
and carried our sorrows;
yet we esteemed him stricken,
smitten by God, and afflicted.
Isaiah 53:4 (ESV)

Jesus went out, bearing his own cross,
to the place called The Place of a Skull,
which in Aramaic is called Golgotha.
John 19:17 (ESV)

Neno la Jumamosi, 12. Aprili 2014

Hizi ndizo amri alizozitangaza
BWANA kwa sauti kubwa kwa kusanyiko
lenu lote huko mlimani kutoka kwenye moto,
wingu na giza nene, wala hakuongeza cho chote zaidi.
Kisha akaziandika juu ya vibao viwili vya mawe,
naye akanipa mimi.
Kumbukumbu La Torati 5,22

Petro alipokuwa angali ananena,
ghafula, wingu linalong'aa likawafunika
na sauti ikatoka kwenye hilo wingu ikisema,
"Huyu ni mwanangu mpendwa,
ninayependezwa naye sana, msikilizeni Yeye."
Mathayo 17,5

Moses said:

These words the Lord spoke to all your assembly
at the mountain out of the midst of the fire, the cloud,
and the thick darkness, with a loud voice;
and he added no more.
Deuteronomy 5:22

A voice from the cloud said,
This is my beloved Son,
with whom I am well pleased;
listen to him.
Matthew 17:5 (ESV)

Neno la Jumatatu, 14. Aprili 2014

Kwa ajili ya jina lake kuu BWANA hatawakataa watu wake,
kwa sababu ilimpendeza BWANA kuwafanya kuwa wake
mwenyewe.
1 Samweli 12,22

Nilikuchukua toka miisho ya dunia,
nilikuita kutoka pembe zake za mbali, nilisema,
'Wewe ni mtumishi wangu, nimekuchagua wala
sikukukataa.
Isaya 41,9

The Lord will not forsake his people,
for his great name's sake,
because it has pleased the Lord
to make you a people for himself.
1 Samuel 12:22 (ESV)

You are my servant,
I have chosen you and not cast you off.
Isaiah 41:9

Neno la Jumanne, 1. Aprili 2014

Mimi ndimi BWANA, Mungu wako,
nikushikaye mkono wako wa kuume na kukuambia,
"Usiwe na hofu, nitakusaidia."

Isaya 41,13

Kristo asema:

Amani nawaachia, amani yangu nawapa,
amani hii niwapayo si kama ile ulimwengu utoayo.
Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiogope.

Yohana 14,27

I, the Lord your God, hold your right hand;
it is I who say to you,
"Fear not, I am the one who helps you."

Isaiah 41:13 (ESV)

Christ says:

Peace I leave with you; my peace I give to you.
Not as the world gives do I give to you.
Let not your hearts be troubled, neither let them be afraid.

John 14:27 (ESV)

Neno la Alhamisi, 3. Aprili 2014

Wakati Potifa aliposikia kisa hiki mkewe alichomweleza,
akisema,

"Hivi ndivyo mtumwa wako alivyonitenda."
Hasira ya Potifa ikawaka.

Mwanzo 39,19

Yeye alipotukanwa,
hakurudisha matukano,
alipoteswa,

hakutishia, bali alijikabidhi kwa Yeye ahukumuye kwa haki.

1 Petro 2,23

Potiphar's wife had accused Joseph wrongly:

As soon as his master heard the words
that his wife spoke to him,
"This is the way your servant treated me,"
his anger was kindled.

Genesis 39:19

When Christ was reviled, he did not revile in return;
when he suffered, he did not threaten,
but continued entrusting himself to him who judges justly.

1 Peter 2:23 (ESV)

Neno la Jumatano, 30. Aprili 2014

Wapendeni adui zenu, watendeeni mema,
wakopesheni bila kutegemea kurudishiwa mlichokopesha.
Ndipo thawabu yenu itakapokuwa kubwa,
nanyi mtakuwa wana wa Aliye Juu,
kwa sababu Yeye ni mwema kwa watu wasio na shukrani
na waovu.

Luka 6,35

Sasa nimewekewa taji ya haki ambayo Bwana,
mwamuzi wa haki, atanitunukia siku ile, wala si mimi tu,
bali pia wote ambao wamengoja kwa shauku kuja Kwake.

2 Timotheo 4,8

Love your enemies, and do good,
and lend, expecting nothing in return,
and your reward will be great,
and you will be sons of the Most High,
for he is kind to the ungrateful and the evil.

Luke 6:35 (ESV)

Henceforth there is laid up for me
the crown of righteousness,
which the Lord, the righteous judge,
will award to me on that Day,
and not only to me
but also to all who have loved his appearing.

2 Timothy 4:8 (ESV)

Neno la Jumatatu, 28. Aprili 2014

Akatufanya sisi kuwa ufalme na makuhani,
tumtumikie Mungu Wake ambaye ni Baba yake.
Utukufu na uwezo vina Yeye milele na milele! .

Ufunuo wa Yohana 1,6

Mtaitwa makuhani wa BWANA,
mtaitwa watumishi wa Mungu wetu.

Isaya 61,6

Jesus Christ made us a kingdom,
priests to his God and Father,
to him be glory and dominion forever and ever.

Revelation 1:6 (ESV)

You shall be called the priests of the Lord;
they shall speak of you as the ministers of our God.

Isaiah 61:6 (ESV)

Neno la Jumamosi, 5. Aprili 2014

Utakuwa taji ya fahari mkononi mwa BWANA,
taji ya kifalme mkononi mwa Mungu wako.
Isaya 62,3

Wazee wa kanisa wanaoongoza
shughuli za kanisa vizuri wanastahili heshima mara mbili,
hasa wale ambao kazi yao ni kuhubiri na kufundisha.
1 Timotheo 5,17

You shall be a crown of beauty in the hand of the Lord,
and a royal diadem in the hand of your God.
Isaiah 62:3

Let the elders who rule well
be considered worthy of double honor,
especially those who labor in preaching and teaching.
1 Timothy 5:17 (ESV)

Neno la Jumatatu, 7. Aprili 2014

Niliwapa mgongo wangu wale wanipigao,
mashavu yangu wale wang'oao ndevu zangu,
sikuuficha uso wangu kutokana na fedheha na kutemewa
mate.
Isaya 50,6

Kristo hakutenda dhambi, wala udanganyifu haukuonekana
kinywani mwake. Yeye alipotukanwa, hakurudisha
matukano,
alipoteswa, hakutishia, bali alijikabidhi kwa Yeye
ahukumuye kwa haki.
1 Petro 2,22-23

I gave my back to those who strike,
and my cheeks to those who pull out the beard;
I hid not my face from disgrace and spitting.
Isaiah 50:6 (ESV)

Christ committed no sin,
neither was deceit found in his mouth.
When he was reviled, he did not revile in return;
when he suffered, he did not threaten,
but continued entrusting himself to him who judges justly.
1 Peter 2:22-23 (ESV)

Neno la Jumamosi, 26. Aprili 2014

Kwa maana kwa moyo mtu huamini na hivyo kuhesabiwa
haki,
tena kwa kinywa mtu hukiri na hivyo kupata wokovu.
Warumi 10,10

Imeandikwa, "Niliamini, kwa hiyo nimesema."
Kwa roho yule yule wa imani pia tuliadini na hivyo
tukasema.
2 Wakorinto 4,13

With the heart one believes and is justified,
and with the mouth one confesses and is saved.
Romans 10:10 (ESV)

Since we have the same spirit of faith
according to what has been written,
"I believed, and so I spoke,"
we also believe, and so we also speak.
2 Corinthians 4:13 (ESV)

Neno la Alhamisi, 24. Aprili 2014

BWANA Mungu wenu amewabariki na amewalinda
Kwa miaka hii arobaini BWANA Mungu wenu amekuwa
pamoja nanyi
na hamkupungukiwa na kitu cho chote.
Kumbukumbu La Torati 2,7

Paulo akaandika:
Mungu wangu atawajaza ninyi kila mnachohitaji kwa
kadiri ya utajiri Wake katika utukufu ndani ya Kristo Yesu.
Wafilipi 4,19

These forty years the Lord your God has been with you.
You have lacked nothing.
Deuteronomy 2:7 (ESV)

Paul writes:
My God will supply every need of yours
according to his riches in glory in Christ Jesus.
Philippians 4:19 (ESV)

Neno la Jumatano, 9. Aprili 2014

Furahini pamoja na wenye kufurahi, lieni pamoja na wale waliao.

Warumi 12,15

Wakumbukeni wale waliofungwa
gerezani kama vile nanyi mmefungwa pamoja nao.

Waebrania 13,3

Rejoice with those who rejoice,
weep with those who weep.

Romans 12:15 (ESV)

Remember those who are in prison,
as though in prison with them.

Hebrews 13:3 (ESV)

Neno la Ijumaa, 11. Aprili 2014

kwa maana yote yanayoweza kujulikana
kumhusu Mungu ni dhahiri kwao,
kwa sababu Mungu mwenyewe ameliweka wazi kwao.

Warumi 1,19

Tazama jinsi kilivyo kina cha
utajiri wa hekima na maarifa ya Mungu!
Tazama jinsi ambavyo hukumu Zake,
hazichunguziki na ambavyo njia Zake zisivyotafutikana!

Warumi 11,33

Wat can be known about God is plain to men,
because God has shown it to them.

Romans 1:19

Oh, the depth of the riches
and wisdom and knowledge of God!
How unsearchable are his judgments
and how inscrutable his ways!

Romans 11:33 (ESV)

Neno la Jumanne, 22. Aprili 2014

Ndipo yule bwana akamwambia mtumishi wake,
"Nenda kwenye barabara na vijia
vilivyoko nje ya mji na uwalazimishe
watu waingie ili nyumba yangu ipate kujaa."

Luka 14,23

Lakini mhitaji hatasahaulika siku zote,
wala matumaini ya walioonewa hayatapotea.

Zaburi 9,18

The master said to the servant,
Go out to the highways and hedges
and compel people to come in,
that my house may be filled.

Luke 14:23 (ESV)

The needy shall not always be forgotten,
and the hope of the poor shall not perish forever.

Psalms 9:18

Neno la Jumapili, 20. Aprili 2014

Masikio yangu yalikuwa yamesikia habari zako,
lakini sasa macho yangu yamekuona. Kwa hiyo najidharau
mwenyewe na kutubu katika mavumbi na majivu.

Ayubu 42,5-6

Ghafula nuru kutoka mbinguni ikamwangaza kote kote.
Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia,
"Sauli, Sauli, mbona unanitesa?"
Sauli akajibu, "U nani wewe, Bwana?"
Ile sauti ikajibu, "Mimi ni Yesu unayemtesa".

Matendo ya Mitume 9,3-5

I had heard of you by the hearing of the ear,
but now my eye sees you;
therefore I despise myself,
and repent in dust and ashes.

Job 42:5-6 (ESV)

Suddenly a light from heaven flashed around Saul.
And falling to the ground he heard a voice saying to him,
"Saul, Saul, why are you persecuting me?"
And he said, "Who are you, Lord?"

And he said, "I am Jesus, whom you are persecuting."

Acts 9:3-5 (ESV)

Neno la Jumapili, 13. Aprili 2014

Kwa kuwa hutia jeraha,
lakini pia huyafunga, huumiza, lakini mikono yake pia
huponya.
Ayubu 5,18

Akasema,
“Aba, Baba, mambo yote yawezekana Kwako.
Niondolee kikombe hiki, lakini si kama nitakavyo Mimi,
bali mapenzi Yako yatimizwe.”
Marko 14,36

God wounds, but he binds up;
he shatters, but his hands heal.
Job 5:18 (ESV)

Jesus said, Abba, Father,
all things are possible for you.
Remove this cup from me.
Yet not what I will, but what you will.
Mark 14:36 (ESV)

Neno la Jumanne, 15. Aprili 2014

BWANA ataniokoa, nasi tutaimba kwa vyombo vya
nyuzi siku zote za maisha yetu katika hekalu la BWANA.
Isaya 38,20

Neno la Kristo lidumu kwa wingi ndani yenu,
mkifundishana na kuonyana katika hekima yote,
mkimwambia Mungu zaburi, nyimbo na tenzi za
rohoni huku mkiwa na shukrani mioyoni mwenu.
Wakolosai 3,16

The Lord will save me,
and we will play my music on stringed instruments
all the days of our lives, at the house of the Lord.
Isaiah 38:20 (ESV)

Let the word of Christ dwell in you richly,
teaching and admonishing one another in all wisdom,
singing psalms and hymns and spiritual songs,
with thankfulness in your hearts to God.
Colossians 3:16 (ESV)

Neno la Ijumaa, 18. Aprili 2014

Je, binadamu aweza kuwa mwadilifu kuliko Mungu?
Je, mtu aweza kuwa safi kuliko Mwumba wake?
Ayubu 4,17

Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti,
bali karama ya Mungu ni uzima
wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.
Warumi 6,23

Can mortal man be in the right before God?
Can a man be pure before his Maker?
Job 4:17 (ESV)

The wages of sin is death,
but the free gift of God is eternal life
in Christ Jesus our Lord.
Romans 6:23 (ESV)

Neno la Jumatano, 16. Aprili 2014

Jinsi gani kijana aifanye njia yake kuwa safi?
Ni kwa kutii akilifuata neno lako.
Zaburi 119,9

Paulo amwandikia Filemoni:
Sikuzote ninamshukuru Mungu ninapokukumbuka katika
maombi yangu.
Filemoni 1,4

How can a young man keep his way pure?
By guarding it according to your word.
Psalms 119:9

Paulus writes to Philemon:
I thank my God always
when I remember you in my prayers.
Philemon 1:4 (ESV)